



NISHATI

HABARI ZA
NISHATI

News *Bulletin*


www.nishati.go.tz [Wizara ya Nishati](#) [wizara_ya_nishati_tanzania](#) [@Nishati2017](#) [Wizara ya Nishati](#)

Toleo Namba 33

Desemba 1 - 31, 2021

MIAKA 60 YA UHURU NA MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI

**>>> SOMA
TAARIFA YA
KINA KUHUSU
MAFANIKIO
SEKTA YA
NISHATI
NDANI YA
MIAKA 60 YA
UHURU UK
WA 3 HADI 11**



Waziri wa Nishati, January Makamba



**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti
Mhandisi Leonard Masanja
Katibu Mkuu

Makamu Mwenyekiti
Kheri Mahimbali

Mhariri
Dorina G. Makaya

Waandishi

Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar

Msanifu Kurasa

Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu
namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma



 www.nishati.go.tz

 [Wizara ya Nishati](#)

 [@Nishati2017](#)

 [wizara_ya_nishati_tanzania](#)

 [Wizara ya Nishati](#)

MIAKA 60 YA UHURU NA MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI

➤ Sekta ya Nishati ina historia ndefu kuanzia kipindi cha kabla ya kupata Uhuru wetu mwaka 1961 hadi kufikia kipindi hiki cha kuadhimisha miaka 60 ya Uhuru wa Taifa letu. Sekta hii imepitia maadiliko mbalimbali ya kimuundo, kisheria na kisera yakiwa na lengo la kuiboresha Sekta hii ili iweze kutoa huduma bora kwa watazania. Wizara inayosimamia Sekta ya Nishati kwa mara ya kwanza iliundwa mwaka 1961 na iliitwa Wizara ya Biashara, Madini na Nguvu za Umeme, hata hivyo sekta ya nishati imekuwa ikitenganishwa au kuunganishwa na kuunda Wizara mbalimbali kutokana na mahitaji ya wakati husika.

➤ Majina ya Wizara zilizohusisha sekta ya nishati kwa nyakati mbalimbali ni Wizara ya Biashara, Madini na Nguvu za Umeme (1961 – 1963); Wizara ya Viwanda, Madini na Nguvu Za Umeme (1963 -1965); Wizara ya Maji na Nguvu za Umeme (1970 – 1975); Wizara ya Maji, Nishati na Madini (1975 – 1980); Wizara ya Maji na Nishati (1980 - 1984); Wizara ya Maji, Nishati na Madini (1984 - 1985); Wizara ya Nishati na Madini (1985 - 1990); Wizara ya Maji, Nishati na Madini (1990 - 1995); Wizara ya Nishati na Madini (1995 – 2017); na Wizara ya Nishati (2017 mpaka Sasa).

➤ Mawaziri waliowahi kuongoza Wizara zinazohusu Sekta ya Nishati ni: Bw. A. H. Jamal, Bw. J. S. Kasambala, Bw. A. Z. Nsilo Swai, I. Elinawinga, Dkt. W. K. Chagula, Bw. Alnoor Kassum,



Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba akisoma kwa Waandishi wa Habari (hawapo pichani) taarifa ya mafanikio sekta ya nishati ndani ya miaka 60 ya Uhuru kwa niaba ya Waziri wa Nishati, January Makamba.

Bw. John Samwel Malecela, Bw. Jackson Makweta, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete, Dkt. William Shija, Bw. Edgar Diones Maokola Majogo, Dkt. Abdallah Omari Kigoda, Bw. Daniel Yona, Bw. Ibrahim Msabaha, Bw. Nazir Mustapha Karamagi, Bw. William Mganga Ngeleja, Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Bw. George Simbachawene, Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Dkt. Medard Matogoro Kalemami na Waziri wa sasa ni Mhe. Bw. January Makamba.

➤ Mawaziri Wadogo ambao wamewahi kutumika kumaanisha cheo cha sasa

cha Naibu Waziri. Manaibu Waziri waliowahi kuongoza Wizara zinazohusu Sekta za Nishati na Madini ni: Bw. J. A. Mhaviile, Bw. K. H. Ameir, Bw. Al-Noor Kassum, Bw. Mustapha C. Nyang'anyi, Bw. Manju Msambya, Bw. Edgar Diones Maokola Majogo, Meja Jakaya Mrisho Kikwete, Mhe. Ernest K. Nyanda, Mhe. Joseph F. Mwiliza, Bw. Benard Membe, Bw. Lawrence Masha na Bw. William Mganga Ngeleja, Bw. Adam K. A. Malima, Bw. George Simbachawene, Bw. Steven Masele, Bw. Charles Kitwanga, Bw. Charles Mwijage, Dkt. Medard Kalemami, Bi. Subira Mgalu na Naibu Waziri wa

MIAKA 60 YA UHURU NA MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI

sasa ni Mhe. Wakili Stephen Byabato.

- Makatibu Wakuu waliowahi kuongoza Wizara zinazohusu Sekta za Nishati na Madini ni: Bw. H. Halwenge, Bw. Jacob Dickson Namfua, Bw. Amon James Nsekela, Bw. Frederick Kilibata Lwegarulila, Bw. Harith Bakari Mwapachu, Bw. Athumani Iddi Janguo, Bw. Samweli Rwakatare, Bw. Fulgence Michael Kazaura, Bw. Paul. J. Mkanga, Prof. Mark Mwandosya, Dkt. Ben Moshi, Bw. Rafael O. S. Mollel, Dkt. Jonas P. Kipokola, Bw. Patrick Rutabanzibwa, Bw. Arthur G. K. Mwakapugi, Bw. David Kitundu Jairo, Bw. Eliakim Maswi, Prof. Justin Ntalikwa, Dkt. Hamisi Mwinyimvua, Mha. Zena Said na Katibu Mkuu wa sasa ni Mha. Leonard R. Masanja.

➤ Dira na Dhima kama

Dira

Kuwa taasisi yenye ufanisi na inayojali tija ili kuhakikisha kuwa rasilimali za nishati zinachangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi kijamii na kiuchumi.

Dhima

Kuendeleza, kudhibiti na kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za nishati kwa manufaa ya Watanzania.

➤ Malengo

Wizara ya Nishati imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Mpango Mkakati wa

Wizara wenye malengo makuu sita (6) kama ifuatavyo:

- i) Kuongeza uzalishaji wa umeme na kuboresha mifumo ya usafirishaji na usambazaji wa umeme;
- ii) Kuongeza mchango wa nishati jadidifu katika matumizi mbalimbali ya nishati;
- iii) Kuimarisha shughuli za utafiti na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia;
- iv) Kuboresha rasilimali za Wizara ili kutoa huduma bora za nishati;
- v) Kutekeleza kwa ufanisi Mkakati wa Taifa wa Kupambana na Kuzuia Rushwa; na
- vi) Kupunguza maambukizi ya VVU na UKIMWI sehemu za kazi na kuboresha utoaji wa huduma kwa waathirika.

- Majukumu ya Wizara ni Kusimamia Sekta ya Umeme na Nishati Jadidifu na Sekta ya Mafuta na Gesi.

➤ SEKTA YA UMEME NA NISHATI JADIDIFU

Mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Umeme na Nishati Jadidifu ni pamoja na:

- 1) **Kuongezeka kwa uzalishaji wa umeme nchini.** Hadi kufikia Mwezi Septemba, 2021 upatikanaji wa umeme umefikia **MW 1,609.91 ikilinganishwa na MW 17.5** kabla ya Uhuru. Mahitaji ya juu ya umeme nchini (*peak demand*) yamefikia **MW 1,273.42** mwezi Oktoba, 2021. Uwezo wa mitambo

ya kufua umeme iliyoungwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa umefikia **MW 1,573.65** ambapo umeme wa nguvu ya maji (36.46%); gesi asilia 57.28%; Mafuta (5.60%); na Tungamotaka (Biomass) (0.67%). Uwezo wa mitambo hiyo unajumuisha mitambo inayomilikiwa na TANESCO ambayo huchangia (86.57%) na mitambo ya wazalishaji binafsi (IPPs/SPPs) ambayo huchangia (13.43%).

Uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme iliyopo nje ya Gridi ya Taifa (*off-grid*) ni **MW 36.26** ambapo TANESCO inamiliki mitambo yenye **MW 32.21** na mzalishaji binafsi NextGen Solawazi (Kigoma) **MW 5** kwa kutumia nguvu ya jua.

- 2) **Kukamilika kwa mitambo ya kuzalisha umeme kwa nguvu ya maji ya: Hale MW 21** (mwaka 1964) na njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kV 11 kutoka Hale hadi Dar es salaam; Nyumba ya Mungu **MW 8** (mwaka 1968) na njia ya umeme ya msongo wa kV 66 Kutoka nyumba ya Mungu hadi Arusha; Kidatu **MW 204** (mwaka 1975- 1981); Mtera **MW 80** (mwaka 1988); New Pangani Falls **MW 68** (mwaka 1995); na kihansi wa **MW 180** (mwaka 2000).

- 3) **Kukamilika kwa ujenzi wa mitambo ya kufua umeme kwa kutumia gesi asili ya: Songas MW 189** (mwaka 2004); Ubungo I **MW 102** (mwaka 2008); Ubungo II **MW 105** (mwaka 2012); Tegeta **MW 45** (mwaka 2009); Somanga

MIAKA 60 YA UHURU NA MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI

Fungu **MW 7.5** (mwaka 2010); Kinyerezi I **MW 150** (mwaka 2016) na ujenzi wa njia za umeme wa kV 220 (Kinyerezi - Kimara) na kV 132 (Kinyerezi - Gongolamboto); Nyakato **MW 63** (mwaka 2013), Kinyerezi II **MW 248** (mwaka 2018) na Mtwara gas power plant **MW 22** (mwaka 2019).

- 4) **Kukamilika kwa ujenzi wa njia za kusafirisha umeme** za: kV 66 yenye urefu wa Kilomita 125 kutoka Mbala, Zambia hadi Sumbawanga (mwaka 2001); kV 220 kutoka Singida na Arusha (mwaka 1996) km 300; kV 132 kutoka Ubungo-Makumbusho (mwaka 2010) kilomita 7; kV 132 yenye urefu wa kilomita 80 kutoka Mtwara hadi Mahumbika (Lindi) pamoja na vituo vya kupoza umeme vya Mtwara na Mahumbika; kV 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga kupitia Dodoma na Singida km 670 (mwaka 2016), kV 220 kutoka Makambako hadi Songea km 250 pamoja na ujenzi wa vituo vitatu (3) vya kupoza umeme vya Makambako, Madaba na Songea (mwaka 2018); na kV 220 Bulyanhuku Geita km 55 (mwaka 2020).
- 5) Kuendelea na Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu za: (REA I, REA II na REA III) na ambao umewezesha vijiji **8,897** kupatiwa umeme kati ya vijiji vyote **12,345** na kubakia na vijiji 3,448 visivyokuwa na huduma ya umeme; Kuendelea kuunganisha umeme wateja wapya nchini kwa kasi ambapo hadi Juni, 2021 jumla ya

Watanzania wanaotumia nishati ya umeme wameongezeka kufikia takriban milioni 47 sawa na asilimia 78 ya Watanzania wapatao milioni 60.

- 6) **Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vipya vya kupoza umeme kwa ajili ya kuboresha upatikanaji na umeme** vya Mbagala, Kipawa, Gongolamboto na Mburahati Mkoani Dar es Salaam; vituo vya kupoza umeme vya Njiro B, Mount Meru, Sakina, Unga Ltd, Kiltex na Themi Mkoani Arusha; vituo vya kupoza umeme vya Bomambuzi na Trade School Mkoani Kilimanjaro; ukarabati wa vituo vya kupoza umeme vya Mikocheni, Oysterbay, City Centre, Gongolamboto, Kariakoo, Mbagala, Chang'ombe, Kipawa na Ubungo Mkoani Dar es Salaam.
- 7) **Kukamilika kwa ujenzi wa vituo vipya vya kupoza umeme** vya Mbagala, Kipawa, Gongolamboto na Mburahati Mkoani Dar es Salaam; Njiro B, Mount Meru, Sakina, Unga Ltd, Kiltex na Themi Mkoani Arusha; Bomambuzi na Trade School Mkoani Kilimanjaro; Kukamilika kwa ukarabati wa vituo vya kupoza umeme vya Mikocheni, Oysterbay, City Centre, Gongolamboto, Kariakoo, Mbagala, Chang'ombe, Kipawa na Ubungo Mkoani Dar es Salaam; kukamilika kwa kituo cha kupoza umeme

cha Dege, Kigamboni 132/33 kV pamoja na njia ya kV 132 toka Kibada hadi Dege.

- 8) **Kukamilika kwa ujenzi wa njia za msongo wa kV 33, kV 11 na kV 0.4 kwa ajili ya kusambaza umeme katika Mikoa ya Dodoma, Iringa, Manyara, Mbeya, Morogoro, Mwanza, Njombe na Tanga kwa ufadhili wa Millenium Challenge Corporation (MCC).**
- 9) **Kukamilika kwa mradi wa kusambaza umeme wa Electricity V (2015)** katika Wilaya za Bukombe, Kwimba, Magu, Mbogwe, Misungwi na Sengerema. Mradi huo ulihusu ujenzi wa njia ya kusambaza umeme wa Msongo wa kV 33, kufunga transfoma na kuwaunganisha umeme wateja 8,600.
- 10) **Kujengwa na kukamilika "submarine cable"** mbili zilizopita chini ya bahari zenye msongo vya Kilovoti 132 na kV 33 kwenda Visiwa vya Unguja na Pemba kV33 sawia.
- 11) **Kukamilika mradi wa ORIO** katika Miji ya Ngara, Biharamulo na Mpanda ambao umeimarisha upatikanaji wa umeme katika miji hiyo.
- 12) **Kukamilika kwa Sera, Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Nishati:** Sera ya Taifa ya Nishati 1992, 2003 na 2015, Sheria ya Umeme ya Mwaka 2008 na mabadiliko yake ya Mwaka 2020, Sheria ya Wakala

MIAKA 60 YA UHURU NA MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI

wa Nishati Vijijini (2005), Sheria ya Mamlaka ya kuthibiti na Huduma za Nishati na Maji, (2001); Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Umeme (*Power System Master Plan*) wa Mwaka 2008, 2012, 2016 na 2020, Mkakati na Mwelekeo wa Maboresho katika Sekta Ndogo ya Umeme (*Electricity Supply Industry Reform Strategy and Action Plan (2014 – 2025)*), Programu ya Nishati Endelevu kwa Wote (*Sustainable Energy for ALL (SE4ALL) Action Agenda 2015*), Programu ya Umeme Vijijini (*Rural Electrification Programu*) 2016 na Mpango Kabambe wa Matumizi ya Gesi Asilia (*Natural Gas Utilization Master Plan – NGUMP*) 2016.

- 13) **Kukamilisha kwa Kanuni (Rules) mbalimbali kwa ajili ya Udhibiti huduma za nishati.** Kanuni hizo ni pamoja na: Kanuni za Uendelezaji na Usimamizi wa Miradi Midogo ya Umeme (*The Electricity (Development of Small Power Projects) Rules, 2016, GN No. 217 of 2016*); Kanuni za Tozo na Ada za Leseni za Umeme (*The Electricity (Licensing Fees) Rules, 2016, GN No. 287 of 2016*); Kanuni za Usimamizi wa Mifumo ya Umeme (*The Electricity (System Operation Services) Rules, 2016, GN No. 324 of 2016*); Kanuni za Usimamizi wa Soko la Biashara ya Umeme (*The Electricity (Market Operation Services) Rules, 2016, GN No. 325 of 2016*); Kanuni za kusimamia Uuzaji umeme (*The Electricity (Supply Services) Rules, 2017, GN No. 4 of 2017*); na Usimamizi

wa Biashara ya Rejareja ya Petrolu Vijijini na kwenye Miji Midogo (*The Petroleum (Retail Operations in Townships and Villages) Rules, 2017, GN No. 14 of 2017*).

- 14) **Kuongezeka kwa kiwango cha upatikanaji umeme nchini.** Kiwango cha upatikanaji wa umeme kwa ujumla (*overall electricity access level*) Tanzania Bara kimeongezeka na kufikia **asilimia 78.4**, ambapo mijini (*urban electricity access level*) imefikia **asilimia 99.6** na vijijini (*rural electricity access level*) takriban **asilimia 69.8**.
- 15) **Kuongezeka kwa idadi ya Taasisi zilizopatiwa umeme vijijini.** Hadi kufikia mwezi Machi, 2020 jumla ya Taasisi na maeneo ya umma 15,200 yamepatiwa umeme chini ya Mpango wa REA ambapo taasisi za elimu (4,036), maeneo ya biashara (5,053), visima/mashine za maji (338), taasisi za afya (1,296) na nyumba za ibada (1,113).
- 16) **Kuandaliwa na kuanza kutumika kwa mikataba mahsusi ya kuuziana umeme** (*Standardized Power Purchase Agreement - SPPA*) kwa wawekezaji wadogo inayotoa mwongozo wa bei (*Standardized Power Purchase Tariff - SPPT*), ambapo wawekezaji watano (5) - (TANWAT-MW 2.75, TPC-MW 20, Sao Hill-MW 16, Ngombeni-MW 0.5 na Mwenga-MW 3.36), wamepewa leseni za kuzalisha umeme wenye jumla ya MW 42.61.

- 17) **Kukamilika kwa Mradi wa kuboresha Mfumo wa Usambazaji Umeme katika Jiji la Dar es Salaam.** Mradi ulihusisha: ukarabati wa Kituo cha Ilala kV 132/33/11; ujenzi wa Jengo Jipya la "Control Center" la Ilala; ufungaji wa njia ya pili ya usafirishaji umeme wa Msongo wa kV 132 kutoka Ubungo hadi Ilala; kupanua Kituo cha kupoza umeme cha Msasani kV 33/11; ujenzi wa Vituo Vipya vinne (4) vya kupoza umeme wa kV 33/11 vya Jangwani Beach, Mwananyamala, Msasani na Muhimbili; ujenzi wa njia mpya za Msongo wa kV 33 kutoka Vituo vya kupoza umeme vya Makumbusho, City Centre na Tegeta kwenda Vituo Vipya vya Mwananyamala, Muhimbili, Jangwani na Msasani;
- 18) **Kukamilika kwa utekelezaji wa Programu ya Awamu ya Pili ya Mradi wa Sustainable Solar Market Package (SSMP – II) (2016).** Mradi ilihusu ujenzi wa Mifumo ya Umeme Jua katika Wilaya nane (8) za Biharamulo, Bukombe, Chato, Kasulu, Kibondo, Namtumbo, Sikonge na Tunduru na kufungwa Jumla ya Mifumo Midogo ya Umeme 4,620 yenye uwezo wa kWp 115.
- 19) **Kuunganishwa kwa Mikoa katika Gridi ya Taifa.** Hadi kufikia Mwezi Septemmba, 2021 mikoa yote ya Tanzania Bara ilikuwa imeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa isipokuwa mikoa minne tu ya Kigoma, Katavi, Rukwa; baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Kagera. Hata hivyo, Mkoa na Kagera

MIAKA 60 YA UHURU NA MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI

wanapata umeme kutoka nchi za Zambia na Uganda sawia.

20) **Kusitisha matumizi ya mitambo ya kukodi** ya binafsi ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta mazito katika kuzalisha umeme ikiwemo ya Aggreko na IPTL na kuokoa wastani wa jumla ya **Shilingi bilioni 11.46** kwa mwezi.

21) **Kusitisha uingizaji wa vifaa vya ujenzi wa miundombinu ya umeme** ikiwemo nguzo, transfoma, nyaya na mita za LUKU ndani ya nchi na Kuendelea na kuhamasisha uzalishaji wa vifaa vya kuunganisha umeme hapa nchini na kuokoa wastani wa **Shilingi bilioni 162.57** kwa mwaka.

22) **Kugunduliwa kwa maeneo yanayoweza kuzalisha umeme kutokana na jotoardhi** katika maeneo ya Songwe (Mbeya), Ziwa Manyara (Manyara), Maziwa Eyasi na Natron (Arusha), Luhoi (Rufiji-Pwani), ambapo takriban kati ya MW 150 – 650 zinaweza kuzalishwa, hivyo kuongeza vyanzo vya nishati nchini.

23) **Kuwezesha matumizi ya umeme** wa jua katika maeneo ya huduma za kijamii kama zahanati, shule za sekondari na taa za barabarani katika wilaya ya Sumbawanga vijijini kupitia mradi mkubwa wa umeme wa jua (*Sustainable Solar Market Packages*).

➤ **Mafaniko mengine kwa upande wa Sekta ya Umeme na Nishati Jadidifu ni:**

(i) Kuendelea na Ujenzi wa Mradi wa kimkakati wa Julius Nyerere Hydro Power Project (JNHPP) MW 2,115 ambao hadi mwezi Septemba, 2021 ulikuwa umefika **asilimia 45.58**; Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Rusumo MW 80 ambao hadi Mwezi Septemba umefikia **asilimia 82** na kuanza maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya kufua umeme ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222);

(ii) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kusafirisha umeme ikiwemo: kV 400 Julius Nyerere Hydro Power Project – Chalinze; kV 400 Singida – Arusha – Namanga; kV 220 Geita – Nyakanazi; kV 220 Rusumo – Nyakanazi; kV 220 kwa ajili ya Uendeshaji wa Treni ya Mwendo Kasi (SGR) Awamu ya Kwanza kutoka Dar es salaam hadi Morogoro na kV 220 kilomita 160, Morogoro – Dodoma – Singida (SGR II), kV 400 kutoka Iringa – Mbeya – Tunduma hadi Sumbawanga kilomita 624; kV 400 kutoka Nyakanazi hadi Kigoma kilomita 280; kV 132 yenye urefu wa kilomita 53.8 kutoka Malagarasi hadi Kidahwe Mkoani Kigoma;

(iii) Kuendelea na utekelezaji wa Mradi wa Rusumo MW 80 ambao hadi sasa utekelezaji wake umefikia **asilimia 82** na kuanza maandalizi ya utekelezaji wa miradi ya kufua umeme ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222);

(iv) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kusafirisha umeme ikiwemo: kV 400 Julius

Nyerere Hydro Power Project – Chalinze; kV 400 Singida – Arusha – Namanga; kV 220 Geita – Nyakanazi; kV 220 Rusumo – Nyakanazi;

(v) Kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kuunganisha gridi ya Taifa na nchi za jirani ambapo utekelezaji wa miradi ya Singida – Arusha – Namanga kV 400 wa kuunganisha nchi za Tanzania na Kenya, Iringa – Mbeya – Tunduma kV 400 wa kuunganisha nchi ya Tanzania na Zambia, na mradi wa Rusumo – Nyakanazi kV 220 utawezesha kuunganishwa kwa nchi za Tanzania, Rwanda na Burundi; na

(vi) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme katika maeneo yaliyo pembezoni mwa miji yaani vijiji-miji (peri-urban). Jumla ya wateja 32,568 kati ya 37,713 wanaotarajiwa kuunganishwa w a m e s h a u n g a n i s h w a . Aidha, maeneo/vijiji/mitaa iliyopelekewa umeme ni 226 kati ya 227 inayotarajiwa kupelekewa umeme.

SEKTA YA MAFUTA NA GESI

➤ Kabla ya uhuru biashara ya mafuta ilianza maeneo ya mwambao wakati Bw. Smith MacKenzie alipoanza kuingiza mafuta kwenye visiwa vya Zanzibar kama wakala wa Kampuni ya Shell. Kampuni hiyo ilipanua shughuli zake hadi maeneo ya Tanzania Bara na pia ilijihusisha na utafutaji wa mafuta hadi mwaka 1964.

➤ Mwaka 1966, Serikali kwa

MIAKA 60 YA UHURU NA MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI

kushirikiana na kampuni ya Agip iliunda kampuni ya Tanzania and Italian Petroleum Refinery (TIPER) ambayo ilihusika na kuagiza, kusafisha na kuuza mafuta kwa kampuni za usambazaji. Hata hivyo, kiasi cha mafuta kilichokuwa kinasafishwa na kampuni hiyo hakikukidhi mahitaji. Kutokana na sababu hiyo, mwaka 1969 Serikali ilianzisha Shirika la Maendeleo ya Petrolini nchini (TPDC), chini ya Sheria ya Mashirika ya Umma ya mwaka 1969 iliyotolewa kwenye *Government Notice* Na. 140 ya tarehe 30 Mei, 1969 na kuanza rasmi shughuli zake mwaka wa fedha 1973/74. TPDC pia ilikuwa na jukumu la kusimamia shughuli za utafiti wa awali na utafutaji mafuta kwa kushirikiana na kampuni nyingine chini ya mikataba ya *Production Sharing Agreement* (PSA).

- Serikali ilitoa leseni ya utafutaji wa mafuta ya petroli kwa Kampuni ya AGIP katika eneo la mwambao wa bahari ya Hindi kutoka Mtwara hadi Tanga. Shughuli za utafutaji wa mafuta zilianza rasmi mwaka 1973 na kampuni hiyo ikagundua gesi asilia katika eneo la Songo Songo mwaka 1974. Kwa kuwa lengo lilikuwa ni kupata mafuta, AGIP ilirudisha eneo hilo kwa Serikali mwaka 1975 na kuendelea na utafutaji wa mafuta. Wakati AGIP ikiendelea na juhudi za utafutaji mafuta, TPDC ilianza rasmi shughuli za uagizaji mafuta ghafi mwaka 1977. Mwaka 1980, Sheria ya Utafutaji na Uendelezaji wa

Mafuta (Petroleum Exploration and Production Act, 1980) ilitungwa ili kuwezesha mikakati ya Serikali ya kuhamasisha ushiriki wa kampuni za kimataifa. Mwanzoni mwa miaka ya 1980, Serikali iliingia mikataba ya utafutaji (PSA) na kampuni za Shell, ELF, AMOCO na International Energy Development of America. Mwaka 1982, Kampuni ya AGIP iligundua tena gesi asilia katika eneo la Mnazi Bay na kurudisha eneo hilo kwa Serikali. Kwa upande wa mafuta, Serikali kupitia TPDC ilikuwa na utaratibu wa kuagiza mafuta ghafi na kuyasafisha nchini katika kiwanda cha TIPER. Kwa kuwa kiasi cha mafuta kilichosafishwa nchini hakikukidhi mahitaji, TPDC ilianza kuagiza mafuta yaliyosafishwa Mwaka 1983.

- Mwaka 1984-1989, shughuli za utafutaji mafuta ziliongezeka baada ya TPDC kuanza kushiriki kikamilifu kwa kufanya kazi za kuchimba visima sita vya utafiti katika mwambao na kina kirefu cha bahari katika maeneo ya Songo Songo visima vitatu (3), Kimbiji visima viwili (2) na kisima kimoja (1) katika kina kirefu cha bahari.
- Utafiti uliofanyika mwaka 1990 ulionyesha kuwa eneo la Songo Songo lina hifadhi ya gesi asilia kiasi cha futi za ujazo bilioni 540. Aidha, gesi hiyo ilionekana kuwa na ubora wa hali ya juu kwa kuwa na kiasi kikubwa cha gesi ya *methane*, kutokuwa na *sulphur* na kuwa na kiasi kidogo cha maji. Serikali kupitia TPDC

iliingia mikataba na kampuni ya mafuta ya India (ONGC) ya kuchimba visima vitatu katika eneo hilo ili kuhakiki kiasi cha gesi asilia kilichopo.

- Kutokana na kuwepo kiasi kikubwa cha gesi asilia, Serikali ilibuni mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asili (*Songo-Songo Gas to Electricity Project*). Lengo la Serikali lilikuwa kutekeleza mradi huu kwa kutumia wawekezaji binafsi ili kuepuka madhara yanayoweza kutokea katika ujenzi na uendeshaji. Mwaka 1994, kupitia utaratibu wa ushindani, Serikali iliichagua Kampuni ya Ocelot Energy Inc. na TransCanada Pipelines Ltd (OTC) consortium kufanya upembuzi yakinifu wa mradi wa Songo-Songo. Mikataba kati ya Serikali na Kampuni hiyo wa kuendeleza mradi ulisainiwa mwezi Oktoba, 1995. Kwa upande mwingine, Serikali ilifanya majadiliano na kampuni za World Wide Exploration (Australia), Dublin International Petroleum Ltd (Ireland), Kisoa (Dubai) na Hunt United (USA) kwa ajili ya utafutaji mafuta na gesi kwenye maeneo yaliyotarajiwa kupitishwa bomba la gesi. Kampuni hizo hazikuweza kugundua chochote.
- Mwaka 1996-2000 Serikali ilianzisha taratibu za kuwa na soko huria katika biashara ya mafuta ili kuleta ushindani ambao utarahisisha upatikanaji na unafuu wa bei za mafuta na bidhaa zake. Pamoja na kuanzishwa kwa soko huria

MIAKA 60 YA UHURU NA MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI

bei za mafuta ziliendelea kupanda kiholela na kuleta adha kwa watumiaji. Kufuatia hali hiyo, mwaka 2006 Serikali iliunda Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (Energy and Water Utilities Regulatory Authority-EWURA).

- Kuanzishwa kwa Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, kuanzishwa kwa Taasisi ya Mdhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), kuwepo kwa Kanuni za utekelezaji kama vile za Bei ya Gesi Asilia, Ushirikishwaji wa Wazawa (Local Content Regulations), Ukusanyaji wa Tozo zitokanazo na mauzo ya gesi asilia (Annual levy – Fee and Charges), kumeimarisha utekelezaji, usimamizi na uendeshaji wa shughuli za utafutaji mafuta na uzalishaji gesi asilia hapa nchini. Usimamizi wa sekta umezidi kuimarika baada ya kuwepo Sheria na Kanuni hizi ambazo zimeandaliwa na kupitishwa ndani ya miaka mitano, kuanzia mwaka 2015 hadi 2020.
- Serikali iliweka mikakati ya kuhamasisha ushiriki wa wazawa katika shughuli za mafuta na gesi na hadi kufikia mwaka 2015 idadi ya wazawa iliongezeka maradufu katika kazi za utafutaji mafuta na gesi na uzalishaji wa gesi asilia. Kwa mfano, idadi ya wazawa walio Shiriki katika uchimbaji wa kisima cha Kitatange-1 katika bahari kuu mwaka 2016 walikuwa nane (8), wakati wazawa wapatao 58 kati ya wafanyakazi 160 waliokuwepo, walishiriki katika

uchimbaji wa kisima cha Pilipili-1 kilicho chimbwa katika bahari kuu mwaka 2018. Idadi ya wazawa walioajiriwa na kuchukuwa nafasi mbalimbali za uongozi katika Makampuni ya kigeni yanayotekeleza shughuli za utafutaji na uzalishaji gesi asilia hapa nchini imeongezeka. Kwa mfano, Katika kampuni la Statoil na Shell, idadi ya wazawa walioajiriwa katika nafasi za uongozi walikuwa chini ya asilimia 50%, wakati kwa mwaka 2020 imefika zaidi ya asilimia 90%.

- Katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015, Kampuni ya Mafuta ya Taifa (TPDC) imeanza kushiriki moja kwa moja katika utafutaji wa mafuta katika eneo la Eyasi Wembere lililopo katika Mikoa ya Tabora, Manyara na Simiyu kwa kutumia wataalamu wa ndani. Katika eneo la Eyasi Wembele, TPDC imefanikiwa kuchoronga visima viwili (2) vifupi (shallow borehole) vya utafiti wa awali, na inatarajia kuchoronga kisima kimoja (1) mwanzoni mwa Mwezi July 2020, hivyo kupelekea kuwa na jumla ya visima vitatu (3) katika eneo hilo. Pia, kwa sasa TPDC ipo katika maandalizi ya kuchoronga visima vya utafutaji wa mafuta na gesi katika Kitalu cha Mnazi Bay Kaskazini.

Mafanikio katika Sekta ya Mafuta na Gesi

- Tangu kupatikana kwa uhuru, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuiwezesha Sekta Mafuta na

Gesi iweze kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya nchi. Katika kipindi hicho mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwa ni pamoja na:

- (a) Kugunduliwa kwa gesi asili katika maeneo ya Songo Songo (1974); Mnazi bay (mwaka 1982), Mkuranga (mwaka 2007), Kiliwani Kaskazini (mwaka 2008) na Kina Kirefu cha Bahari (mwaka 2010). Aidha, gesi iliyogunduliwa nchi kavu na kina kirefu cha bahari ni Futi za Ujazo **Trilioni 57.54** mwaka 2021. Ugunduzi huo umewezesha kuanza kutumika kwa gesi asilia kama chanzo cha nishati, hususan kwa kuzalisha umeme, viwandani, majumbani na kwenye magari.
- (b) Hadi mwezi Oktoba, 2021, viwanda **52** Jijini Dar es Salaam, Mkoani Pwani na Mtwara vinatumia gesi asilia. Aidha, vituo viwili vya kushindilia na kujazia gesi asilia kwenye magari jijini Dar es Salaam na Mtwara vinafanya kazi.
- (c) Matumizi ya gesi asilia yamesaidia kupunguza utegemezi wa uzalishaji umeme kwa kutumia nguvu za maji ambapo hadi Novemba, 2021 takribani **asilimia 60** ya umeme unazalishwa kwa kutumia gesi asilia.
- (d) Katika kipindi cha mwaka 2004 hadi Juni, 2020 matumizi ya gesi asilia ya Mnazi Bay na Songo Songo yamesaidia Serikali kuokoa zaidi ya **Shilingi Trilioni 38** ambazo zingetumika kwa ajili ya ununuzi wa mafuta

MIAKA 60 YA UHURU NA MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI

ya mitambo ya umeme na ya viwandani.

(e) Hadi mwezi Machi, 2021 mapato yanayotokana na mauzo ya gesi yamechangia zaidi ya **Shilingi bilioni 208** katika Mfuko wa Mafuta na Gesi kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 baada ya kukamilika Ujenzi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Mtwara/ Songosongo hadi Dar es Salaam.

(f) Hadi mwezi Desemba, 2020 Serikali imepata mapato ya zaidi ya **shilingi bilioni 441** yanayotokana na kodi mbalimbali kuanzia mwaka 2015 baada ya kukamilika kwa mradi wa Bomba la Kusafirisha Gesi Asilia kutoka Mtwara/ Songosongo hadi Dar es salaam.

(g) Shirika la Maendeleo ya Mafuta nchini (TPDC) limelipa zaidi ya **shilingi bilioni 10** katika mwaka 2018/2019 na mwaka 2019/20 ikiwa ni gawio (Dividend) kwa Serikali.

(h) Hadi Juni, 2021 zaidi ya **Magari 750** yamewekewa mfumo wa matumizi ya nishati ya gesi asilia.

(i) Kuanzishwa na kuendelea kuimarika kwa Mfumo wa Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja (Bulk Procurement System – BPS) ambao umeongeza uhakika wa upatikanaji wa mafuta nchini na kupunguza gharama za uagizaji. Kuanzishwa kwa mfumo wa Bulk Procurement System (BPS) umeleta mafanikio

mbalimbali ikiwemo:

(j) Upatikanaji wa mafuta yanayotosheleza mahitaji ya nchi na yenye viwango vya ubora unaotakiwa wakati wote (security of supply);

(k) Kupata unafuu wa gharama za uletaji mafuta (premium) nchini kutokana na uagizaji; wa pamoja (economies of scale) ambapo takribani **shilingi bilioni 462** huokolewa kila mwaka ikilinganishwa na kabla ya mfumo husika kuanza kutumika

(l) Kuwezesha Serikali kupanga ukusanyaji wa mapato kwa kuzingatia takwimu sahihi, kwani kumerahisisha katika kupanga/kufanya Makadirio ya Mapato ya kodi yatokanayo na mafuta yanaoyingizwa nchini; na

(m) Kupungua kwa gharama za meli kusubiria nafasi ya kushusha mafuta (Demurrage Charges) kutokana na upangaji mzuri wa meli katika mfumo wa BPS, kwa sasa meli husubiria hadi siku 8 ikilinganishwa na siku 60 kabla ya mfumo wa BPS. Aidha, **takribani bilioni 391** huokolewa kila mwaka ikilinganishwa demurrage zilizokuwa zikilipwa kabla ya mfumo wa BPS.

(n) Kuanzishwa kwa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu (PURA) ambapo kumewezesha kuongezeka kwa ushiriki wa Watanzania (Local Content) katika shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli na kuimarika

kwa Shughuli za Kaguzi za Gharama katika Mikataba ya PSAs (PSA Audit) ambapo kwa sasa kati ya PSA kumi (10) zilizofanyiwa ukaguzi, mbili (2) zimekamilika hadi mwaka 2020 na nane (8) zimekamilika hadi mwaka 2019. Kaguzi hizi hadi sasa zimewezesha kuokoa fedha takribani **shilingi bilioni 35.91**.

(o) Kuanzishwa kwa udhibiti wa huduma za nishati chini ya EWURA kumesaidia kuhakiki bei za bidhaa za mafuta. Aidha, upangaji wa bei elekezi (*indicative price*) na bei kikomo (*cap price*) katika biashara ya mafuta ya jumla na rejareja unafanyika kupitia mamlaka hiyo. Hatua hii imezingatia maslahi ya mtumiaji na muuzaji.

(p) Kuongezeka kwa ushiriki wa Watanzania katika miradi ya mafuta na gesi asilia ambapo hadi kufikia mwezi Oktoba 2021 zaidi ya kampuni 1,000 zimeorodheshwa katika kanzidata inayomilikiwa na EWURA ikishirikiana na PURA iliyowezesha kampuni hizo kushiriki katika miradi mbalimbali.

(q) Kuanza kwa shughuli za utafutaji wa mafuta katika Kitalu cha Eyasi Wembere ambapo visima vifupi vitatu (3) vyenye kina cha urefu wa mita 300 vimechorongwa katika eneo la Kining'inila Wilayani Igunga (Tabora), Nyalanja wilayani Meatu (Shinyanga) na Luono wilayani Iramba (Singida);

(r) Kuanzishwa kwa Mradi Wa

MIAKA 60 YA UHURU NA MAFANIKIO KATIKA SEKTA YA NISHATI

Kuchakata Na Kusindika Gesi Asilia (Liquefied Natural Gas - LNG). Mradi huu unalenga kuvuna, kuchakata na kusindika gesi asilia iliyogunduliwa kwenye kina kirefu cha Bahari ya Hindi katika Vitalu namba 1, 2 na 4 kuwa kimiminika ili iweze kuuzwa nje ya nchi na kutenga kiasi kingine kwa matumizi ya soko la ndani.

- (s) Kuhuishwa kwa Bandari za Tanga na Mtwara katika kupokea Mafuta ambapo Bandari hizo zimeanza kupokea Mafuta kuanzia mwezi Julai, 2015 na Julai, 2018 mtawalia.
- (t) Kujenga uwezo katika kusimamia Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa kudhamini mafunzo ya ufundi stadi kupitia vyuo vya ufundi stadi (VETA). Serikali imeendelea kutoa kozi mbalimbali zinazohusiana na mafuta na gesi katika vyuo vikuu hapa nchini kwa viwango vya Stashahada (Diploma), Shahada (Bachelor) na Uzamili (Masters).
- (u) Kupungua kwa uchafuzi (uchakachujaji) wa mafuta kutoka wastani wa **asilimia 19.2** mwaka 2015 hadi kufikia wastani wa **asilimia 4** mwezi Machi, 2020.
- (v) Kuanzishwa kwa Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi Kutoka Uganda Hadi Tanzania (East African Crude Oil Pipeline - EACOP). Mradi unaohusisha ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi (crude oil) lenye urefu wa Kilomita 1,443 kutoka Kabaale

nchini Uganda hadi Mkoani Tanga. Gharama za mradi zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani bilioni 3.55 ambazo ni takriban **Shilingi trilioni 8.1. Hadi sasa Serikali imewezesha** Kusainiwa kwa Mkataba kati ya Nchi Hodhi na Wawekezaji (*Host Government Agreement – HGA*); Kusainiwa kwa Mkataba wa Ubia baina ya Wawekezaji (*Shareholders' Agreement – SHA*); Kukamilika kwa majadiliano na kuridhiwa kusainiwa kwa Mikataba ya uendeshaji wa Bandari ya Chongoleani na Mikataba ya ukodishaji wa ardhi ya mradi kwa maeneo ya kipaumbele na mkuza wa bomba; Kukamilika kwa malipo ya fidia kwa eneo la Chongoleani itakapojengwa Bandari; Kuendelea na ulipaji wa fidia kwa Wananchi wanaopisha ujenzi wa mradi; Utoaji wa elimu kwa wananchi katika maeneo yanayopitiwa na mradi ni kazi endelevu; na Kusainiwa kwa mkataba wa nchi zinazotekeleza mradi (Intergovernmental Agreement-IGA).

- (w) Kuendeleza Ushirikiano baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) kupitia Wizara zinazohudumu katika sekta ya Nishati kwa kutilia mkazo ushirikiano wa masuala ya umeme, na mafuta na gesi.
- (x) Kuanzishwa kwa Miradi ya kimkakati ya usafirishaji wa Gesi Asili kwenda Kenya na Uganda. Miradi hii ipo katika hatua za awali za majadiliano

na kukamilika kwake kutaleta manufaa katika kusambaza gesi asili maeneo mradi utakapopita kwa Tanzania; Serikali kupata fedha za kigeni kutokana na mauzo ya gesi katila nchi husika; na kuimarisha uhusiano wa kidiplomasia na nchi za Kenya na Uganda.

- (y) Kuwezesha ujenzi wa vituo vya mafuta vya gharama nafuu katika maeneo mbalimbali ya vijijini ili kuimarisha usalama na upatikanaji wa huduma bora za mafuta katika maeneo hayo.
- (z) Kuongezeka kwa matumizi ya nishati ya kisasa ikiwemo gesi ya mitungi (Liquefied Petroleum Gas - LPG) kwa ajili ya kupikia katika maeneo ya mijini na vijijini.

HITIMISHO

Sekta ya Nishati ni miongoni mwa sekta muhimili katika kukuza na kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Mwelekeo wa Sekta hii katika kipindi cha miaka ijayo ni kuhakikisha kuwa inaendelea kuchangia kwa kiwango kikubwa katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya Taifa, kuondoa umaskini na kuboresha maisha ya Watanzania. Hivyo, Wizara inadhamiria kuendelea kujiimarisha zaidi kiutendaji kwa lengo la kuzidi kuiimarisha Sekta hii ili iweze kutoa mchango stahiki kwa maendeleo ya Taifa letu.

Waziri Makamba aingia katika doria

Waziri wa Nishati, January

Makamba, amefanya doria katika mito inayoingiza maji katika mabwawa ya vituo vyote vya kuzalisha umeme kwa nguvu ya maji.

Katika doria hiyo, Waziri Makamba aliambata na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Umeme Tanzania, Maharage Chande na maafisa wengine wa Shirika hilo. Doria hiyo ililenga kutathmini hali ya ukame katika mito hiyo, kiwango cha maji katika mabwawa, hali ya uzalishaji katika vituo hivyo, na kutathmini hatua za kuchukua kukabiliana na hali hiyo.

Waziri Makamba alishuhudia mtiririko hafifu katika Mto Ruaha na kukauka vya mito midogo inayochangia katika mtiririko wa mto Ruaha na katika bwawa dogo la Kidatu.

Hali hiyo imesababishwa na ukame mkali unaotokana na kutonyesha mvua katika maeneo yanayolisha mito hiyo na pia matumizi mabaya ya rasilimali-maji na



Waziri wa Nishati, January Makamba akiwa katika chumba cha kuongozea mitambo katika moja ya vituo vya kuzalisha umeme kwa nguvu ya maji.

uharibifu wa mazingira katika maeneo husika.

Hali hii imesababisha upungufu wa Megawati 307 kati ya Megawati 561 zinazopaswa kuzalishwa kutokana na nguvu ya maji. Waziri Makamba pia alipata nafasi ya kuzungumza na wafanyakazi katika vituo vya kuzalisha umeme, pamoja na wananchi na viongozi mbalimbali katika maeneo hayo.

Akizungumza na wafanyakazi wa TANESCO na viongozi mbalimbali katika maeneo husika, Waziri Makamba alisema kwamba ni dhahiri kwamba kuna ukame mkubwa ambao umeathiri mtiririko wa

maji na hivyo kuathiri uzalishaji wa umeme. Alisisitiza umuhimu wa hifadhi ya mazingira na matumizi ya rasilimali-maji yanayozingatia Sheria mbalimbali za nchi na hifadhi ya mazingira.

Alisema kwamba TANESCO na Serikali zinachukua hatua za muda mfupi, wa kati na muda mrefu kukabiliana na upungufu wa umeme. Mkurugenzi Mkuu wa TANESCO, Ndugu Maharage Chande, aliongeza kwamba Shirika linachukua hatua za haraka kuongeza uzalishaji kwa kutumia gesi asilia, kwa kuharakisha matengezo

ya baadhi ya mitambo yake ya Ubungo I (MW 25), Upanuzi wa Kinyerezi I (MW 185) na Ubungo III (MW 112). Aidha, Shirika limelazimika kuwasha kituo cha kuzalisha umeme cha Nyakato (MW 36).

Hatua hizi zitakazokamilika kwa hatua kuanzia Desemba, 2021 hadi Machi, 2022 zitasaidia kuongeza jumla ya MW 350 katika mfumo wa gridi ya Taifa. Shirika pia linaendelea na matengenezo na maboresho ya mfumo wa usambazaji na ugavi wa umeme ikiwemo kuharakisha maboresho ya miundombinu ya kusafisha umeme ya

Waziri Makamba aingia katika doria

220kV Kidatu – Iringa, 220kV Kingolwira – Msamvu na vituo vya kusambazumeme vya Msamvu, Luguruni, Kunduchi na Nyakanazi. Pia, TANESCO itafanya maboresho katika njia za kasambaza umeme ambazo kwa sasa ni ndefu nazinapeleka wateja kupata umeme hafifu (low voltage) na uharibifu wa mara kwa mara wa mita.

Waziri Makamba aliilekeza TANESCO kuhakikisha kwamba, pamoja na kadhia hii ya umeme, Shirika lisijiingize kwenye kukodi mitambo ya dharura kutokana na historia mbaya ya mitambo ya aina hiyo kuwa na gharama kubwa kwa Serikali na kugubikwa na utata mwingi.

Badala yake,

amelielekeza Shirika kuhakikisha kwamba linaongeza miradi mipya ya uzalishaji umeme kwa njia ya upepo na jua ambayo inaweza kutekelezwa ndani ya mwaka mmoja ili mwakani katika kipindi kama hiki cha umeme taifa lisikabiliwe tena na uhaba wa umeme.

Pia ameelekeza kwamba TANESCO, kama msimamizi wa mradi

wa kufua umeme wa Mwalimu Nyerere kule Rufiji, ihakikishe kwamba mradi huo hauchelewi kwa kiwango kikubwa ili nao uchangie katika majawabu ya kudumu ya upatikanaji wa umeme nchini.

Waziri Makamba aliwasihi wananchi wawe na subira katika kipindi hiki kigumu wakati TANESCO ikihakikisha kwamba inadhibiti

upungufu wa uzalishaji kwa njia mbalimbali. “Nimeingia katika nafasi hii katika siku 70 tu zilizopita, wajibu wangu ni kumsadia Rais wetu Mhe Samia Suluhu Hassan, na kuisaidia nchi yetu, kwa kuisimamia TANESCO ipasavyo ili itemize wajibu wake na tuondokane na kadhia hii haraka iwezekanavyo”, alisema Waziri Makamba.



PICHA mbalimbali zikimwonesha Waziri wa Nishati, January Makamba akifanya doria katika mito inayoingiza maji katika mabwawa ya vituo vyote vya kuzalisha umeme kwa nguvu ya maji.

Waziri Makamba aanzisha Majadiliano Mradi wa LNG



Waziri wa Nishati, January Makamba akizungumza jambo wakati jijini Arusha, alipofungua majadiliano ya utekelezaji wa mradi wa gesi ya kimiminika (Liquefied Natural Gas-LNG) baina ya Serikali na Kampuni za Shell Tanzania ambao ni wawekezaji katika vitalu namba 1 na 4 na Equinor ambao ni wawekezaji katika kitalu namba 2.

Waziri wa Nishati, January

Makamba ameanzisha majadiliano ya utekelezaji wa mradi wa gesi ya kimiminika (Liquefied Natural Gas-LNG) baina ya Serikali na Kampuni za Shell Tanzania ambao ni wawekezaji katika vitalu namba 1 na 4 na Equinor ambao ni wawekezaji katika kitalu namba 2

Akizungumza mara baada ya kufungua



Watendaji kutoka Wizara na Taasisi za Serikali wakimsikiliza Waziri wa Nishati, January Makamba jijini Arusha, wakati akifungua majadiliano ya utekelezaji wa mradi wa gesi ya kimiminika (Liquefied Natural Gas-LNG) baina ya Serikali na Kampuni za Shell Tanzania ambao ni wawekezaji katika vitalu namba 1 na 4 na Equinor ambao ni wawekezaji katika kitalu namba 2.

kikao cha majadiliano jijini Arusha, Waziri Makamba alisema “Serikali imedhamiria kwa dhati kuendeleza shehena kubwa ya gesi asilia iliyogundulika katika kina kirefu cha bahari kwa kuwa na mradi wa LNG ambao utawezesha kuivuna na kuiuza gesi hiyo kwa soko la kimataifa na pia kuhudumia mahitaji yetu ya ndani na yale ya kanda”.

Waziri Makamba aliongeza kuwa mradi wa LNG ni miongoni mwa miradi mikubwa ya kimkakati inayotekelezwa na Serikali kupitia Wizara ya Nishati ambapo mradi huu unakadiriwa kugharimu shilingi Trilioni 70 za Kitanzania na kuzalisha ajira zaidi 7000.

Kwa upande wao Wawakilishi wa Makampuni ya Shell na Equinor, Bi. Uni Fjær ambaye ni Mkurugenzi Mkazi wa Equinor Tanzania na Ndg. Jared Kuehl ambaye ni Mkurugenzi Mkazi kutoka kampuni ya Shell walieleza utayari wa makampuni yao kutekeleza mradi huu mkubwa kwa maslahi ya pande zote. Bi. Uni alisema “Equinor ina dhamira ya dhati kuona mradi huu unatekelezeka

Waziri Makamba aanzisha Majadiliano Mradi wa LNG

kwa wakati kwa faida ya pande zote”.

Naye Ndg. Jared kutoka Shell alisema “ Shell pamoja wabia wake inafuraha kuona majadiliano ya kutekeleza mradi wa

LNG yameanza tena na tunaamini kwa pamoja tutafikia malengo tuliyojiwekea”

Mradi wa LNG unahusisha uvunaji wa gesi iliyogunduliwa baharini na kuibadili

kuwa kimiminika ili kuweza kuisafirisha kwa urahisi kwa ajili ya kuuza katika masoko ya kimataifa na sehemu ya gesi hiyo pia itatumika kuhudumia mahitaji ya ndani na yale ya Kanda

ya Afrika Mashariki na Kati. Mradi huu utajengwa Mkoani Lindi ambapo Serikali kupitia TPDC tayari ilishatwaa eneo na kulipa fidia wananchi katika eneo hili tayari kwa kuanza kutekeleza mradi pale majadiliano yatakapokamilika.



Watendaji kutoka kampuni ya Shell na Equinor wakimsikiliza Waziri wa Nishati, January Makamba jijini Arusha, wakati akifungua majadiliano ya utekezaji wa mradi wa gesi ya kimiminika (Liquefied Natural Gas-LNG) baina ya Serikali na Kampuni za Shell Tanzania ambao ni wawekezaji katika vitalu namba 1 na 4 na Equinor ambao ni wawekezaji katika kitalu namba 2.

Kampuni ya CNOOC yasaini Mkataba wa Wanahisa wa EACOP

Kampala, Uganda

Kampuni ya Mafuta ya Taifa ya China (CNOOC) ambayo ni mmoja kati ya wanahisa wanne wanaotekeleza mradi wa EACOP, ametia saini mkataba wa wanahisa (Shareholders Agreement) leo Novemba 4, 2021 hatua inayofungua ukurasa mpya wa kuanzisha

>>> Hatua hii itawezesha Kampuni ya Mradi kuundwa

Kampuni maalumu ya Mradi (EACOP Company) ambayo ndio itatekeleza na kuendesha mradi wa EACOP. Wanahisa wengine wa mradi wa EACOP ni pamoja na TPDC (15%), Kampuni ya Taifa ya Mafuta Uganda (UNOC-15%), Total Energies (62%) na

CNOOC (8%).

Akizungumza mara baada ya tukio hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC Dkt. James Mataragio alisema “Leo hii tumeshuhudia hatua nyingine kubwa katika mradi wa EACOP ambapo mmoja ya mwanahisa mwenzetu, CNOOC

amesaini mkataba wa wanahisa na hivyo kuwezesha uanzishwaji wa kampuni ya mradi ambayo ndio itakuwa na jukumu la kutekeleza, kusimamia na kuendesha mradi wa EACOP”. Dkt. Mataragio alieleza kuwa wanahisa wengine wa mradi waliweka sahihi mikataba yote ikiwemo wa wanahisa mnamo Aprili 11, 2021 lakini kampuni ya CNOOC



Rais wa Kampuni ya CNOOC, Ndg. Chen Zhubiao (wapili kutoka kulia waliokaa) akitia saini Mkataba wa Wanahisa wa mradi wa EACOP huku wanahisa wengine wakishuhudia, kutoka kulia waliokaa ni Mkurugenzi kutoka UNOC Ndg. Francis Nagimesi, Mkurugenzi Mtendaji wa TOTAL EACOP, Ndg. Martin Tiffen, na Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio. Wengine waliosimama ni watumishi kutoka TPDC, UNOC na CNOOC.

Kampuni ya CNOOC yasaini Mkataba wa Wanahisa wa EACOP



Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi wa kilomita 1,443 (kati ya hizo kilomita 1,147 ziko nchini Tanzania) za bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda kupitia Tanzania hadi Bandari ya Tanga kwa lengo la kuuza mafuta hayo katika soko la Kimataifa.”

ilihitaji muda zaidi kukamilisha taratibu za kupata idhini kutoka katika Serikali yao kabla ya kusaini mkataba wa wanahisa.

Mkataba huo umetiwa saini na Rais wa Kampuni ya CNOOC, Ndg. Chen Zhuobiao na kushuhudiwa na Wakurugenzi Watendaji kutoka kampuni wanahisa wengine pamoja na wawakilishi wao. Akizungumza baada ya kutia sahihi mkataba huo, Ndg. Chen alisema “Tunaelewa ni kwa kiasi gani hatua hii ilikuwa ikisubiriwa na tunayofuraha kwamba Serikali yetu imetoa idhini kwa CNOOC kuwa mwanahisa katika mradi wa EACOP na hivyo kuwahakikishia wanahisa wengine juu ya utayari wa CNOOC kuendelea kama timu moja katika kufikia malengo makubwa ya mradi wa EACOP kwa manufaa ya

watu wa nchi zetu”.

Aidha, Mkurugenzi Mtendaji wa EACOP, Ndg. Martin Tiffen alieleza furaha aliyonayo kufuatia kampuni ya CNOOC kusaini mkataba wa wanahisa. Ndg. Tiffen alisema “Tumekuwa tukiweka malengo kila mwaka ya kufikia maamuzi ya mwisho ya uwekezaji (Final Investment Decision) na kwa kampuni ya CNOOC kusaini mkataba huu leo ni wazi sasa kuwa mradi wa EACOP umekamilisha hatua ya kuwa na wanahisa na hivyo kuanzisha kampuni ya EACOP ambayo sasa itachukua majukumu ya kutekeleza mradi ambayo yamekuwa yakitekelezwa na TOTAL Energies kwa niaba ya wanahisa wengine”.

Kwa upande wa Tanzania, mradi huu umepiga hatua mbalimbali zikiwemo; ulipaji wa fidia kwa watu

351 katika maeneo ya awali, kukamilika kwa uthamini na uhakiki wa watu 9,122 katika mkuza wa mradi ambapo malipo yanatarajiwa kufanyika wakati wowote kuanzia sasa, kukamilika kwa tathmini ya athari za mazingira na stadi za kijiolojia, kijiofizikia na kijiotekniki katika maeneo ya bahari pamoja na kusainiwa kwa mikataba yote muhimu ya mradi.

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi wa kilomita 1,443 (kati ya hizo kilomita 1,147 ziko nchini Tanzania) za bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima, Uganda kupitia Tanzania hadi Bandari ya Tanga kwa lengo la kuuza mafuta hayo katika soko la Kimataifa. Kwa upande wa Tanzania bomba hili litapita katika mikoa 8 ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida,

Dodoma, Manyara na Tanga. Vile vile mradi wa EACOP utahusisha ujenzi wa miundombinu mingine nchini Tanzania ambayo ni pamoja na; vituo vinne (4) vyenye pampu kwa ajili kusukuma mafuta; vituo viwili (2) vya kupunguza kasi ya msukumo wa mafuta; kituo cha kuhifadhi mafuta takribani mapipa milioni 2; Gati lenye urefu wa kilomita 2 kutoka kwenye kituo cha kuhifadhi mafuta kuelekea kituo cha kupakia Mafuta; Valvu 53 kwenye maeneo muhimu kwa ajili ya kuzuia au kuruhusu utiririkaji wa Mafuta; Vituo vidogo 15 vya umeme kwa ajili ya kupasha joto bomba; Kilomita 107 za barabara mpya na zilizoboreshwa na kambi kumi na mbili (12) za ujenzi wa Mradi. Kazi zote hizi zitatoa fursa za ajira kwa watanzania ambapo inatarajiwa ajira 10,000 hadi 16,000 zitazalishwa katika kipindi cha hadi miaka minne ya utekelezaji wa mradi, mapato kwa serikali, fursa za Watanzania kutoa huduma kwa zile huduma zilizotengwa mahususi kwa ajili ya Watanzania na faida nyingine nyingi.

MAKAMBA AZISHUKURU NORWAY SWEDEN NA SAUD ARABIA

**Hafsa Omar-
Dar es Saalam**

Waziri wa Nishati, January

Makamba amezishukuru nchi za Norway, Sweden na Saud Arabia kwa mchango mkubwa unayoipatia Tanzania katika kuendeleza sekta ya Nishati.

Aliyasema hayo, Novemba 16, 2021 kwa nyakati tofauti wakati alipokuwa na kikao na mabalozi wa Norway, Sweden na Saud Arabia, katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam.

Akizungumza na mabalozi hao, alisema



Waziri wa Nishati, January Makamba (katikati), wakiwa katika picha ya Pamoja na Balozi wa Norway nchini Tanzania, Balozi Elisabeth Jacobsen (tatu-kushoto) Naibu Balozi wa Norway, Bjorn Midthun (pili-kulia) Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mhandisi Hassan Seif Saidy (pili-kushoto) Mshauri Nishati wa Ubalizi wa Norway, Morten Heide (kwanza-kulia) mara baada ya kumaliza kikao na balozi wa Norway, kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 16, 2021.

nchi hizo zimeendelea kutoa ushirikiano kwa Tanzania kwa kufadhili miradi mbali mbali katika Sekta ya Nishati.

Alieleza kuwa, Serikali

itaendelea kunufaika na fursa mbalimbali zinazotelewa na nchi hizo kwakuwa nchi hizo zipo tayari wakati wowote kufanya kazi na

Serikali ya Tanzania.

Aidha, aliwataka mabalozi hao kuendelea kutoa ushirikiano katika kuendeleza sekta ya nishati ambayo ni



Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akizungumza na Balozi wa Norway nchini Tanzania, Balozi Elisabeth Jacobsen wakati alipokuwa na kikao na balozi huyo katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 16, 2021.



Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akizungumza na Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Balozi Anders Sjoberg wakati alipokuwa na kikao na balozi huyo katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 16, 2021.

MAKAMBA AZISHUKURU NORWAY SWEDEN NA SAUD ARABIA



Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akizungumza na Kaimu Balozi wa Saud Arabia nchini Tanzania, Fahd Al-harbi wakati alipokuwa na kikao na balozi huyo katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 16,



muhimu kwa uchumi wa Tanzania.

Kwa upande wake, Balozi wa Norway, Balozi Elisabeth Jacobsen alisema Tanzania ni nchi ambayo inajulikana kwa historia yake ya kuwa na mashirikiano mazuri kwa mataifa mengine.

Alieleza kuwa uhusiano baina ya nchi mbili hizi umedumu kwa takribani miaka 50 ambapo kwa kuzingatia ushirikiano huo nchi hiyo imefadhili miradi mbalimbali katika sekta Nishati na itaendelea kufadhili katika miradi mbalimbali katika sekta hiyo.

Naye, Balozi wa Sweden, Balozi Anders Sjoberg, ameeleza kuwa nchi yake inajivunia

kuwa sehemu ya maendeleo katika sekta ya Nishati nchini Tanzania, ambapo alieleza kuwa nchi yao imefadhili miradi ya mbalimbali ya umeme kama mradi wa Umeme vijijini, Ujazilizi na miradi mengine ya umeme ambayo muhimu na inawanufaisha watazania wote kwa ujumla.

kwa upande wake, Kaimu Balozi wa Saud Arabia, Fahd Al-harbi, alisema nchi yake itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kukuza na kuendeleza sekta ya nishati nchini kwa muda wowote kwakuwa sekta hiyo ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi.



Picha mbalimbali wakati Waziri wa Nishati, January Makamba alipokutana na kufanya kikao na mabalozi wa Norway, Sweden na Saud Arabia, katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam. Novemba 16, 2021.

MAKAMBA AKUTANA NA BALOZI WA UGANDA



Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akizungumza na Balozi wa Uganda nchini Tanzania, Balozi Richard Kabonero wakati wa mazungumzo yaliyofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 15, 2021.



Balozi wa Uganda nchini Tanzania, Balozi Richard Kabonero (katikati) katibu wa Ubalozi Uganda nchini Tanzania, Comfort Amviko, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sekta Binafsi nchini Francis Nanai wakimsikiliza Waziri wa Nishati (hayupo pichani) wakati wa kikao baina ya Waziri wa Nishati na balozi wa Uganda kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara Nishati jijini Dar es Saalam, Novemba 15, 2021.

Hafsa Omar-Dar Es Saalam

Waziri wa Nishati, January

Makamba amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Uganda nchini Tanzania, Balozi Richard Kabonero.

Mazungumzo hayo, yalifanyika Novemba 15,

2021 katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam.

Katika kikao hicho ambacho walijadili maandalizi ya ziara ya Rais wa Uganda, Yoweri Museveni ambae anatarajiwa kuanza ziara nchini Tanzania hivi karibuni.

Aidha, Makamba alisema kuwa Uhusiano mzuri uliopo baina

hizo nchi hizo mbili umepelekea kurahisisha ujenzi wa Bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) na Marais wa nchi hizo mbili watahakikisha kuwa mradi huo unakamilika.

Pia, alisema mradi wa EACOP ni muhimu sana katika nchi hizo mbili na mpaka sasa upo kwenye hatua nzuri.

“Tunafurahi hatua

kubwa iliyofikiwa katika mradi na tunajua umuhimu wa mradi huu kwa nchi zetu zote mbili,” alisisitiza Waziri Makamba.

Kwa upande wake, Balozi wa Uganda nchini Tanzania, Balozi Richard Kabonero alishukuru Serikali ya Tanzania kwa ushirikiano waliotoa kwa kuhakikisha mradi wa Bomba la mafuta unafanikiwa.



Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akiwa katika picha ya Pamoja na Balozi wa Uganda nchini Tanzania, Balozi Richard Kabonero mara baada ya kumaliza kikao kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara Nishati jijini Dar es Saalam, Novemba 15, 2021.



Kamishna wa Petroli na Gesi, Michael Mjinja (katikati) katibu wa Waziri Danford Mpelumbe wakimsikiliza Waziri wa Nishati, January Makamba (hayupo pichani) kwenye kikao baina ya Waziri wa Nishati na Balozi wa Uganda nchini Tanzania kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara Nishati jijini Dar es Saalam, Novemba 15, 2021.

Usambazaji Gesi majumbani iwe ni kipaumbele-PAC

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, imetoa wito kwa Serikali kuwa, suala la usambazaji gesi majumbani liwe ni la kipaumbele.

Wito huo umetolewa kupitia kwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Naghenjwa Kaboyoka jijini Dar es Salaam mara baada ya ziara ya Kamati hiyo kutembelea miundombinu mbalimbali ya Gesi iliyopo mkoani Mtwara, Pwani na Dar es Salaam.

Alisema kuwa usambazaji wa Gesi hiyo majumbani uzingatie kupeleka nishati hiyo kwenye maeneo yenye watu wengi ili kuweza kupunguza matumizi makubwa ya mkaa ambayo yanapelekea



Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakiwa katika mitambo ya kuchakata Gesi ya Madimba mkoani Mtwara. Wengine ni watendaji kutoka Wizara ya Nishati na TPDC.

ukataji wa miti na hivyo kuleta uharibifu wa mazingira.

Kuhusu ziara ya Kamati hiyo kwenye miundombinu ya Gesi alisema kuwa, Kamati imeona uwekezaji mkubwa uliofanyika na kufurahishwa na jinsi wafanyakazi watanzania wanavyoendesha

na kusimamia miundombinu hiyo kwa ufanisi mkubwa.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio alieleza Kamati hiyo kuwa, kazi ya usambazaji Gesi majumbani inaendelea katika mikoa mbalimbali na kwamba ili gesi

hiyo isambazwe kwa wananchi wengi zaidi, wameanza kukaribisha kampuni binafsi ili ziweze kusambaza nishati hiyo majumbani.

Ziara ya PAC ilikuwa na malengo mbalimbali ikiwemo kuona kama ujenzi wa miundombinu ya Gesi iliyopo inalingana na thamani ya fedha iliyotolewa.

Wajumbe wa PAC walitembelea mitambo ya kuchakata gesi ya Mnazi Bay ambapo Gesi hiyo husafirishwa kwenda Mtwara Mjini ili kuzalisha umeme unaotumika katika mikoa ya Mtwara na Lindi na Gesi nyingine hupelekwa kwenye mitambo ya kuchakata Gesi ya Madimba inayomilikiwa na TPDC.

Aidha, Kamati hiyo pia ilitembelea visima



Baadhi ya mitambo ya kuchakata Gesi ya Madimba mkoani Mtwara.



Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakiwa katika mitambo ya kuchakata Gesi ya Mnazi Bay mkoani Mtwara. Wa Pili kutoka kulia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mhe. Naghenjwa Kaboyoka.

Usambazaji Gesi majumbani iwe ni kipaumbele-PAC



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakiwa katika chumba cha kuongozea mitambo cha Madimba mkoani Mtwara. Aliyekaa ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Naghenjwa Kaboyoka.

vya gesi vitano vilivyopo nchi kavu katika eneo hilo la Mnazi Bay mkoani Mtwara, nyumba zilizounganishwa na Gesi Asilia kwa ajili ya kupikia na matoleo ya Bomba kubwa la Gesi ambayo hupeleka Gesi maeneo mbalimbali ikiwemo kiwanda cha Saruji cha Dangote kilichopo mkoani Mtwara.

Aidha, wajumbe hao wa Kamati walitembelea mitambo ya kuchakata Gesi Asilia iliyopo Madimba yenye uwezo wa futi za ujazo milioni 210 ambapo gesi hiyo baada ya kuchakatwa husafirishwa kwa Bomba kubwa linalotoka eneo hilo mpaka mkoani Dar es Salaam na hivyo kuwezesha gesi hiyo



Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kutembelea mitambo ya kuchakata Gesi Asilia ya Mnazi Bay mkoani Mtwara. Wa Pili kulia ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhe. Naghenjwa Kaboyoka.

kutumika kwa matumizi mbalimbali ikiwemo kuzalisha umeme, kutumika viwandani kwenye magari na majumbani.

Vilevile Wajumbe hao walitembelea vituo vya kupokea Gesi iliyochakatwa vya Somanga mkoani Lindi na Kinyerezi jijini Dar es Salaam.

Viongozi mbalimbali waliohudhuria ziara ya Kamati hiyo ni Kamishna Msaidizi wa Gesi, Mohamed Fakihi, akimwakilisha Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio na Kaimu Meneja Mkuu wa GASCO, Baltazary Mrosso.



Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakiwa katika kituo cha kupokea Gesi cha Kinyerezi jijini Dar es Salaam ambacho husambaza Gesi katika maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye mitambo inayozalisha umeme ya Kinyerezi I na II.



Baadhi ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali wakiwa katika chumba cha kuendesha mitambo katika kituo cha kupokea Gesi cha Kinyerezi jijini Dar es Salaam ambacho husambaza Gesi katika maeneo mbalimbali ikiwemo kwenye mitambo inayozalisha umeme ya Kinyerezi I na II. Wa kwanza kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio.

MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA KUWA SULUHISHO LA UHARIBIFU WA MAZINGIRA-MAKAMBA



Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akizungumza na Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) hapa nchini, Manfredo Fanti, wakati alipokuwa na kikao na balozi huyu katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 17, 2021.

Hafsa Omar- Dar es Saalam

Waziri wa Nishati, January

Makamba amesema kuwa mradi wa kuboresha njia endelevu za matumizi ya Nishati safi ya kupikia utasaidia kulinda mazingira na

itakuwa suluhisho la uharibifu wa Mazingira hapa nchini.

Aliasema hayo, Novemba 17, 2021 wakati akiwa na kikao na Balozi wa Umoja wa Ulaya kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati, zilizopo Jijini Dar es Saalam.

Kikao hicho kilihudhuriwa na

Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Felchesmi Mramba, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio na watalaamu kutoka Wizara ya Nishati na timu kutoka katika Ubalozi wa Umoja wa Ulaya hapa nchini.

Akizungumza na Balozi huyu, aliupongeza

ubalozi huo kwa kazi nzuri ya kuandaa miradi ya Nishati jadidifu ambayo itatoa suluhisho la uharibifu wa mazingira na kuwatoa watanzania kwenye matumizi ya mkaa na kuni.

Ubalozi huo unatarajia kuzindua mradi wa kuboresha njia endelevu za matumizi ya Nishati safi ya kupikia

MATUMIZI YA NISHATI SAFI YA KUPIKIA KUWA SULUHISHO LA UHARIBIFU WA MAZINGIRA-MAKAMBA



Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Felchesmi Mramba (kwanza-kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), James Mataragio (katikati) Katibu wa Waziri, Danford Mpelumbe, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, January Makamba (hayupo pichani) wakati wa kikao na Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) hapa nchini, kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 17, 2021.

hivi karibuni ambao utagharimu Euro milioni 30 ambao utaanza kuzinduliwa katika maeneo ya mjini.

“Nawaahidi nitakuwa

na nyie bega kwa bega kuhakikisha mnafanikiwa katika mradi huo muhimu kwa Taifa letu kwasababu njia peke ya kumaliza matumizi ya

mkaa ni Gesi ya kwenye mitungi (Liquefied Petroleum Gas -LPG),” alisisitiza Makamba.

Aidha, alisema Serikali itahakikisha

inatoa ushirikiano kwa Ubalizi huo ili waweze kufanikisha kwa urahisi miradi yote ya Nishati inayokusudiwa kutekelezwa hapa nchini.

Kwa upande wake, Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) hapa nchini, Manfredo Fanti, amesema kuwa wataendelea kufanya kazi na Serikali ya Tanzania na wapo tayari kuzindua miradi hiyo hivi karibuni.

Alisema, Dhumuni la kubuni mradi hiyo ni kupunguza matumizi ya kuni na mkaa na kuongeza kasi ya matumizi ya Nishati jadidifu katika mikoa ya Dar es Saalam, Morogoro, Pwani na kuendelea na maeneo mengine hapa nchini.



Picha mbalimbali wakati wa kikao cha Waziri wa Nishati, January Makamba na Balozi wa Umoja wa Ulaya (EU) hapa nchini kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 17, 2021.

TANZANIA KUENDELEZA VYANZO VYA NISHATI JADIDIFU



Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akizungumza na Balozi wa Denmark nchini, Mette Norgaard Dissing Spandet, wakati alipokuwa na kikao na balozi huyo katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 18, 2021.

Novemba 18, 2021 wakati akiwa na kikao na balozi wa Denmark nchini Tanzania, kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati, jijini Dar es Saalam.

Akizungumza katika kikao hicho alisema, kutokana na ongezeko la mahitaji wa umeme nchini lazima kuwepo na vyanzo vingi vya uzalishaji wa umeme ambavyo vitasaidia na vitaweza kutosheleza upatikanaji wa umeme nchini.

Aidha, aliwataka wawekezaji wenye uwezo kuwekeza kwenye sekta ya Nishati jadidifu katika maeneo mbalimbali nchini ili kuweza kuongeza uzalishaji wa umeme

Hafsa Omar- Dar es Saalam

Waziri wa Nishati, January

Makamba amesema Tanzania itaendelea kuendeleza vyanzo vya umeme wa Upepo na umeme wa Jua (solar) ili kuwa na vyanzo vingi vya uzalishaji wa umeme nchini.

Aliyasema hayo,



Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Felchesmi Mramba (kwanza-kushoto), Mhandisi Mkuu, Christopher Nyondo (katikati) Katibu wa Waziri, Danford Mpelumbe, wakimsikiliza Waziri wa Nishati, January Makamba (hayupo pichani) wakati wa kikao na Balozi wa Denmark hapa nchini, kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 18, 2021.

TANZANIA KUENDELEZA VYANZO VYA NISHATI JADIDIFU



Waziri wa Nishati, January Makamba (katikati), wakiwa katika picha ya pamoja Balozi wa Denmark nchini, Mette Norgaard Dissing Spandet, (kushoto), Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Felchesmi Mramba (kulia) mara baada ya kumaliza kikao balozi wa Denmark, kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 18, 2021.

nchini.

Pia, aliutaka ubalozi huo, kushirikiana na Tanzania katika

kuwajengea uwezo waatalamu wa hapa nchini katika masuala ya teknolojia ya Nishati

jadidifu.

Vilevile, aliwataka wawekezaji mbalimbali kuanzisha viwanda

vya kutengeneza vifaa ambavyo vitavyotumika kwenye uzalishaji wa Nishati jadidifu, vifaa hivyo ambavyo vitawasaidia watumiaji mbalimbali katika sekta hiyo.

Kwa upande wake, Balozi wa Denmark nchini, Mette Norgaard Dissing Spandet, alisema nchi yake kama mdau mkubwa wa maendeleo wataendelea kushirikiana na Tanzania katika kuendeleza sekta ya Nishati hasa kwa upande wa Nishati jadidifu.

Alisema, kuwa wawekezaji kutoka Denmark wapo tayari kuja kuwekeza nchini katika sekta ya Nishati hususani kwa upande wa kuzalisha umeme kwa kutumia Upepo.



Picha mbalimbali wakati wa kikao cha Waziri wa Nishati, January Makamba na Balozi wa Denmark hapa nchini kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 18, 2021.

Waziri wa Nishati afanya mazungumzo na TotalEnergies



Waziri wa Nishati, January Makamba (wa Pili kushoto) akizungumza katika kikao na kampuni ya TotalEnergies kilichofanyika katika Ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dodoma. Kulia kwa Waziri ni Mohamed Fakihi, Kamishna Msaidizi wa Gesi, na kushoto kwa Waziri ni Kaimu Kamishna Msaidizi wa Nishati Jadidifu, Jacob Mayalla.

Waziri wa Nishati, January

Makamba amekutana na kufanya mazungumzo watendaji wa kampuni

ya TotalEnergies ambayo hujishughulisha uzalishaji na uzaji wa nishati ulimwenguni.

Watendaji hao wakiongozwa na Mkurugenzi Mtendaji wa TotalEnergies Tanzania,

Jean Francois Schoepp walifika Wizara ya Nishati kutambulisha rasmi mabadiliko yaliyofanyika ndani ya kampuni hiyo ambapo kwa sasa badala ya kujikita kwenye mafuta na

gesi pekee, wameanza kujishughulisha na masuala ya nishati jadidifu pia.

Kampuni hiyo ilimweleza Waziri wa Nishati nia ya kuwekeza Tanzania kwenye miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu kama vile Jua na Upepo kutokana na uhakika wa upatikanaji wa vyanzo hivyo vya nishati ya umeme.

Waziri wa Nishati ameleza kampuni kuwa nia ya Serikali ni kuwa na umeme wa uhakika unaotokana na vyanzo mbalimbali ikiwemo Nishati Jadidifu hivyo kinachotakiwa ni kufanya taratibu zitakazowawezesha kufanya uwekezaji huo.



Waziri wa Nishati, January Makamba (wa Pili kushoto) akizungumza katika kikao na kampuni ya TotalEnergies kilichofanyika katika Ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dodoma. Kulia kwa Waziri ni Mohamed Fakihi, Kamishna Msaidizi wa Gesi, na kushoto kwa Waziri ni Kaimu Kamishna Msaidizi wa Nishati Jadidifu, Jacob Mayalla.



Waziri wa Nishati, January Makamba (wa Pili kushoto) akiwa katika kikao na kampuni ya TotalEnergies kilichofanyika katika Ofisi za Wizara ya Nishati jijini Dodoma. Kulia kwa Waziri ni Mohamed Fakihi, Kamishna Msaidizi wa Gesi, na kushoto kwa Waziri ni Kaimu Kamishna Msaidizi wa Nishati Jadidifu, Jacob Mayalla. Wengine katika picha ni Watendaji kutoka kampuni ya TotalEnergies na Wizara ya Nishati.

MAKAMBA AZISHUKURU NORWAY SWEDEN NA SAUD ARABIA

**Hafsa Omar-
Dar es Saalam**

Waziri wa Nishati, January

Makamba amezishukuru nchi za Norway, Sweden na Saud Arabia kwa mchango mkubwa unayoipatia Tanzania katika kuendeleza sekta ya Nishati.

Ameyasema hayo, Novemba 16, 2021 kwa nyakati tofauti wakati alipokuwa na kikao na mabalozi wa Norway, Sweden na Saud Arabia, katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam.



Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akizungumza na Balozi wa Norway nchini Tanzania, Balozi Elisabeth Jacobsen wakati alipokuwa na kikao na balozi huyo katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 16, 2021.

Akizungumza na mabalozi hao, amesema nchi hizo zimeendelea kutoa ushirikiano kwa Tanzania kwa kufadhili miradi mbali mbali katika Sekta ya Nishati.

Alieleza kuwa, Serikali itaendelea kunufaika na fursa mbalimbali zinazotelewa na nchi hizo kwakuwa nchi hizo zipo tayari wakati wowote kufanya kazi na

Serikali ya Tanzania. Aidha, amewataka mabalozi hao kuendelea kutoa ushirikiano katika kuendeleza sekta ya nishati ambayo ni muhimu kwa uchumi wa



Waziri wa Nishati, January Makamba (katikati), wakiwa katika picha ya Pamoja na Balozi wa Norway nchini Tanzania, Balozi Elisabeth Jacobsen (tatu-kushoto) Naibu Balozi wa Norway, Bjorn Midthun (pili-kulia) Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Mhandisi Hassan Seif Saidy (pili-kushoto) Mshauri Nishati wa Ubalozi wa Norway, Morten Heide(kwanza-kulia) mara baada ya kumaliza kikao na balozi wa Norway, kilichofanyika katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 16, 2021.



Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akizungumza na Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Balozi Anders Sjoberg wakati alipokuwa na kikao na balozi huyo katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 16, 2021.

MAKAMBA AZISHUKURU NORWAY SWEDEN NA SAUD ARABIA

Tanzania.

Kwa upande wake, Balozi wa Norway, Balozi Elisabeth Jacobsen amesema Tanzania ni nchi ambayo inajulikana kwa historia yake ya kuwa na mashirikiano mazuri kwa mataifa mengine.

Ambapo ameeleza kuwa uhusiano baina ya nchi mbili hizi umedumu kwa takribani miaka 50 ambapo kwa kuzingatia ushirikiano huo nchi hiyo imefadhili miradi mbalimbali katika sekta Nishati na itaendelea kufadhili katika miradi mbalimbali katika sekta hiyo.

Nae, Balozi wa Sweden, Balozi Anders Sjoberg, ameeleza kuwa nchi yake inajivunia

kuwa sehemu ya maendeleo katika sekta ya Nishati nchini Tanzania, ambapo alieleza kuwa nchi yao imefadhili miradi ya mbalimbali ya umeme kama mradi wa Umeme vijijini, Ujazilizi na miradi mengine ya umeme ambayo muhimu na inawanufaisha watazania wote kwa ujumla.

kwa upande wake, Kaimu Balozi wa Saud Arabia, Fahd Al-harbi, alisema nchi yake itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kukuza na kuendeleza sekta ya nishati nchini kwa muda wowote kwakuwa sekta hiyo ni muhimu katika kukuza uchumi wa nchi.



Waziri wa Nishati, January Makamba (kulia) akizungumza na Kaimu Balozi wa Saud Arabia nchini Tanzania, Fahd Al-harbi wakati alipokuwa na kikao na balozi huyo katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam, Novemba 16, 2021.



Picha mbalimbali wakati Waziri wa Nishati, January Makamba alipokutana na kufanya kikao na mabalozi wa Norway, Sweden na Saud Arabia, katika ofisi ndogo za Wizara ya Nishati zilizopo jijini Dar es Saalam. Novemba 16, 2021.

REA yawafunda Malawi usambazaji wa Umeme Vijijini

**Na Zuena Msuya,
Dodoma,**

Wakala wa Nishati Vijijini (REA)

imewafunda wajumbe kutoka nchini Malawi kuwapa elimu ya namna ambavyo imefanikiwa katika kusambaza Umeme Vijijini.

Mafunzo hayo yalitolewa, Novemba 23, Jijini Dodoma, na Kaimu Mkurugenzi wa REA Mhandisi Jones Olotu.

Mha. Olotu alisema kuwa wakala huo uko tayari kuisaidia nchi ya Malawi katika kuipa ujuzi, maarifa ili ifanikiwe katika kuanzisha Wakala wa Umeme Vijijini nchini kwao.

Aliwaeleza kuwa Kwa Tanzania imefanikiwa katika hilo baada ya Serikali kuona umuhinu wa jambo hilo na kuwekeza fedha nyingi ili kuhakikisha malengo yanatimia.

Na aliwaeleza zaidi kuwa Tanzania iliweka kipaumbele katika jambo hilo na kuhakikisha kuwa linakuwepo katika sera, miongozo, na ilani ya Chama tawala ili kuhakikisha utekelezaji wake unafanikiwa kwa kiasi kikubwa.

Aliwaeleza kuwa

endapo wanania thabiti ya kuanzisha wakala kama huo nchini mwao ni vyema watumia njia zilizorumiwa na nchi zilizofanikiwa kama Tanzania.

Aliongeza kuwa sio tu nchi ya Malawi pekee ambayo imekuja kwa ajili ya kujifunza kuhusu masuala haya ya umeme vijijini bali nchi kama Lesotho nao walikuja na wakapata msaada kama huo.

“Tumefurahishwa sana kwa ujio huu na tungependa wafanikiwe hata zaidi yetu kwa kuanzisha wakala wao kwani tungependa kuwa sehemu ya mafanikio yao, hizi ni jitihada kubwa za Serikali kuweza kuziwezesha Taasisi zake ambazo sasa zinaonesha mfano mkubwa na kuiletea sifa kwa maana ya maendeleo ambayo tumeyafanya”, alisema Mhandisi Olotu.

Miongoni mwa mambo waliyofundishwa Wajumbe hao ni pamoja na masuala ya kisheria, utawala, kuvutia wawekezaji wa ndani na nje pamoja na kuisimamia miradi husika.

Awali kabla kupata mafunzo hayo, wajumbe hao walifika katika Ofisi za Wizara ya Nishati, zilizopo katika Mji wa

Serikali Mtumba na kupokelewa na Kaimu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Petro Lyatuu na kuwaeleza kuwa

Tanzania kupitia Wizara ya Nishati imefurahishwa na imepokea ujumbe huo kutoka nchini Malawi kwa ajili ya kujifunza kuhusu kuanzishwa kwa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) na utekelezaji wa majukumu yake nchini.

Lyatuu alimesema kuwa ujumbe kutoka nchini Malawi ambao umejumuisha wataalamu kutoka Wizara za Nishati na Fedha na kuja nchini kujifunza kuhusu REA ni kielelezo tosha kuwa Serikali ya Tanzania imetimiza azma yake ya kuhakikisha kuwa kila Kijiji kinafikiwa na Umeme pamoja na kuwasha Umeme katika kila kaya kwa lengo la kuchochea Maendeleo.

“Tangu kuanzishwa kwa REA mwaka 2007, wakala umekuwa ukitekeleza majukumu yake na kipindi hicho wenzetu wa Malawi wamepata taaarifa mbalimbali kuhusu wakala na mafanikio ambayo wakala umeyapata kwa kipindi hicho na wameona ni vyema wakaja nchini Kwetu ili kujifunza kuhusu kuanzishwa

kwake, changamoto na mafanikio yake” alisema Lyatuu.

Naye Naibu Mkurugenzi kutoka Wizara ya Nishati nchini Malawi Patrick Silungwe amesema wameichagua Tanzania kuja kujifunza kwa sababu ina mafanikio makubwa katika eneo hilo.

“Sisi kama nchi ya Malawi tumekuwa tukitekeleza katika masuala haya ya umeme vijijini kwa muda sasa Serikalini, lakini baada ya kupata misukosuko ya hapa na pale tukaona ni vyema sasa tuanzishe wakala wa umeme vijijini kama nchi, kwaiyo tulihitaji nchi ambayo tayari ni mfano katika masuala haya ya umeme vijijini na hivyo Tanzania ikajitokeza ya kwanza katika orodha yetu na hivyo tumejifunza vyema na tutaenda kutumia maarifa haya kuanzisha wakala wa umeme kutokana na tulichopata Tanzania” ameongeza.

Katika ziara hiyo ya Siku Tatu wajumbe hao pia walipata fursa ya kutembelea baadhi ya maeneo na kuona namna ambavyo mradi wa REA umetekelezwa na unaoendelea kutekelezwa katika Mkoa wa Dodoma.

REA yawafunda Malawi usambazaji wa Umeme Vijijini



**SPEECH BY HON. JANUARY Y. MAKAMBA (MP)
MINISTER FOR ENERGY ON THE OCCASION OF THE
TANZANIA - UGANDA OIL AND GAS SYMPOSIUM HELD
AT THE JULIUS NYERERE INTERNATIONAL
CONVENTION CENTRE, DAR ES SALAAM, TANZANIA
ON 27TH NOVEMBER 2021, JNICC**

Hon. Dr. Ruth Nankabirwa Ssentumu,
Minister for Energy and Mineral Development, Uganda;

Eng. Leonard Masanja,
Permanent Secretary, Ministry of Energy, Tanzania;

Eng. Irene Bateebe,
**Permanent Secretary, Ministry of Energy and Mineral
Development, Uganda;**

Dr. James Mataragio,
**Managing Director, Tanzania Petroleum Development
Corporation;**

Francis Nanai,
Executive Director, Tanzania Private Sector Foundation;

Francis Kisirinya,
Executive Director, Uganda Private Sector Foundation;

Representatives of Political and Religions Presents;

Distinguished Guests, Ladies and Gentlemen;

Representatives of Political and Religions presents

Symposium Coordinators,

Distinguished Guests,

Ladies and Gentlemen,

Protocol Observed

Invited guests, Ladies and Gentlemen

It gives me much pleasure to welcome you all, **distinguished guests from Tanzania and the entire business community delegation from Uganda** to this important symposium here at the Julius Nyerere International Convention Centre (JNICC) in Dar es Salaam.

Invited Guests, Ladies and Gentlemen

My role today is just to deliver Opening Remarks and set the pace for your discussions regarding the Oil and Gas industry in Tanzania and Uganda, in particular, the EACOP project. For that matter, let me take this opportunity to commend the Tanzania and Uganda Private Sector Foundations, all Official Sponsors and stakeholders who were involved in organizing this Conference and making it happen. This Symposium is very special in the sense that it also coincides with H.E

President Museveni's Three- Day State Visit to Tanzania which begins today. I am equally delighted to let you know that both H.E President Samia Suluhu Hassan and President Yoweri Kaguta Museveni will address this Business Forum tomorrow 28 November, 2021 at the State House here in Dar es Salaam. It goes without saying that this Symposium is a testimony of our strong fraternal ties between our Two countries and seeks to strengthen our co-operation in the Oil and Gas Industry among other areas.

On a special Note, allow me to acknowledge the presence of and congratulate Hon. Dr. Ruth Nankabirwa Ssentumu on her recent appointment as Minister for Energy and Mineral Development in Uganda. Your appointment reflects the confidence both the President of Uganda and the people of Uganda have reposed in you. As my counterpart, I wish you the very best in this role and look forward to working with you and push forward our EACOP and EAC integration agenda.

Invited Guests Ladies and Gentlemen

We are all gathered here to dialogue on the status of our East African Crude Oil Pipeline and particularly, " **Where are We?! .** Therefore, my Opening Remarks will attempt to respond to this question.

As we all know, East Africa Crude Oil pipeline (EACOP) is a project that aims at transporting and exporting the crude oil from Uganda through Tanga Port in Tanzania to the International market. The pipeline system will be the longest-heated pipeline in the world with a total length of 1,443 km. It is designed to have a diameter of 24 inches with transportation capacity of 216,000 barrel of oil per day. This project's cost is estimated to cost **USD 3.55 billion.**

Invited Guests, Ladies and Gentlemen

In implementing EACOP Project, a number of key milestones have been achieved to date. Please allow me to mention a few;

Signing of the Key Project Agreements, this is an important step as both the Project Company and the Governments are putting their commitments in implementation of the Project.

The Inter-Governmental Agreement (IGA) between the Government of the United Republic of Tanzania and the Government of Republic of Uganda provides the intention and commitment to undertake the Project.

The Host Government Agreements between the Project Company and each Government sets the required fiscal and legal regime for the implementation of the project. There is also the Shareholders' Agreement which provides for how the Project will be executed.

Enabling Legislation, The GoT through the HGA agreed to facilitate timely implementation of the project including amending some legislation to enable smooth implementation of the Project. Once again, on 09th November, 2021, the Parliament passed the amendments to support the Project.

Commencements of Physical Works, On 05 November, 2021 the Project Company handed over the Project land to Tanzanian



contractor (Milembe Consult) to start Early Civil Works (ECW). The Contractor has started the mobilization of materials, machinery and preparation of working camps for commencement of work.

The ECW includes the clearance, levelling and fencing the Priority areas in Bukombe, Sojo-Nzega and Igunga. The ECW work is expected to be completed within six (6) months from 5th November, 2021.

Invited Guests, Ladies and Gentlemen

The Government of Tanzania conducted project's awareness campaigns in all eight regions of; Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara and Tanga (at the Regional, District, Ward and Village level). These interventions availed to our communities' opportunities arising out of the Project. In deed, we have sent a strong message to our communities for them to be prepared to grab the opportunities. In overall terms, the engagement was intended to raise awareness on ownership for the project at that level.

Invited Guests, Ladies and Gentlemen

This event today yet gives me pleasure to announce to you that Procurement of Level one contractors for the Project is completed. All 13 contractors, are ready to take their duties immediately after

finalization of some pending engagement formalities. As stated earlier, the Early Civil Work Contractor is on Site.

Invited Guests, Ladies and Gentlemen

Before I conclude, let me acknowledge that this Symposium has been conducted at the right time, where the Project Company and the Level one contractors are about to release tenders for the Local Contractors. As you may be aware, the Reserved Contracts for Local Suppliers/Contractors must be enjoyed by local businesses for both Uganda and Tanzania. Our governments believe in your ability and capacity to seize these opportunities.

Generally, both Governments create an enabling environment for your businesses to flourish. EACOP Project presents yet another opportunity for your businesses to grow.

Invited Guests, Ladies and Gentlemen

Our two Governments, the Government of the United Republic Tanzania and the Government of the Republic of Uganda have a political will and are ready to cooperate with other shareholders to implement this Project. Besides, EACOP Project being a strategic one, it comes with potential benefits to both countries, businesses and our people. Allow me to mention few of these benefits as follows;

- Increase in Foreign Direct Investment (FDI) to both Countries **(Estimated CAPEX 3.55bil)**,
- A new source of Government revenues (taxes, levies and tariff)
- Employment Opportunities
- The project shall provide opportunities for private sector growth
- Establishment of a new infrastructure corridor between Uganda and Tanzania
- At least 200 kms network of new permanent roads will be built, and potentially a further 150 km of upgraded roads in Tanzania

Invited Guests, Ladies and Gentlemen

With these few highlights on the project key milestones and next steps, allow me to now announce that "**THE TANZANIA-UGANDA OIL AND GAS SYMPOSIUM ON THE EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE PROJECT**" is officially opened.

Thanks!

**ASANTENI SANA
WEBALE**

JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



Fika Ofisi ya Mawasiliano,
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au
Wasiliana nasi kwa **simu namba** +255-26-2322018
Nukushi +255-26-2320148

 www.nishati.go.tz

 [Wizara ya Nishati](https://www.facebook.com/Wizara.ya.Nishati)

 [@Nishati2017](https://twitter.com/Nishati2017)

 [wizara_ya_nishati_tanzania](https://www.instagram.com/wizara_ya_nishati_tanzania)

 [Wizara ya Nishati](https://www.youtube.com/Wizara.ya.Nishati)